# HOTUBA YA MGENI RASMI, DKT. JAMES ANDILILE, MKURUGENZI MKUU, MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA), WAKATI WA UFUNGUZI WA MAFUNZO YA KUWAJENGEA UWEZO WAJUMBE WA KAMATI ZA WATUMIAJI ZA MIKOA ZA EWURA CCC, MOROGORO.

**JANUARI 23, 2024**

**Ndugu Mwenyekiti wa Baraza, Mha. David Ngula,**

**Ndugu Wajumbe wa Baraza,**

**Ndugu Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Ndg. Stella Lupimo,**

**Ndugu Wajumbe wa Kamati za Watumiaji za mikoa,**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ndugu Mwenyekiti,** Nami niungane nawe na washiriki wengine wa mafunzo haya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Afya njema, na Baraka ya kukutana hapa kwa ajili ya siku hii muhimu ya kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Watumiaji za mikoa za EWURA CCC.

Nipende pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Baraza kunialika kuwa Mgeni Rasmi kwenye ufunguzi wa mafunzo haya muhimu kwa Wajumbe wa Kamati za mikoa za Baraza ambazo kiukweli zimekuwa zikiliwakilisha vema si tu Baraza bali pia zimekuwa kiungo muhimu kati ya wananchi wanaotumia huduma za nishati na maji, Baraza, Watoa Huduma na hata Mdhibiti. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa, Baraza linakuwa na wawakilishi katika mikoa wenye ufahamu wa kutosha kuhusu majukumu yao.

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo**, Kama ilivyokwisha kuelezwa na Mwenyekiti, Kifungu cha 31 (1)(C) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, imetoa mamlaka kwa Baraza kuanzisha Kamati za Watumiaji za Mikoa na kushauriana nazo. Ni kupitia kifungu hiki, leo hii Wajumbe hawa wanaoanza kupatiwa mafunzo wamepatikana. Nilipongeze Baraza kwa kutekeleza moja ya majukumu yake ya kisheria ya kuanzisha Kamati hizi.

Aidha, nawapongeza sana Wajumbe wote wa Kamati kwa kuteuliwa kutumika na kutumikia wananchi kwenye maeneo mnakotoka. Uteuzi huu unaonesha Imani ambayo Baraza limeendelea kuwa nayo kwenu katika kuliwakilisha na kutekeleza majukumu yake kwenye ngazi ya mikoa, lakini pia kwa upande wenu inaonesha Imani mliyonayo kwenye Baraza na utayari wa kuendelea kutekeleza majukumu ya kuusaidia umma wa watanzania hususani watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo**, kama ilivyoarifiwa awali kuwa Wajumbe wa Kamati hizi za EWURA CCC za mikoa wanatekeleza majukumu yao kwa kujitolea. Lakini pia nimearifiwa na kusikia hapa kuwa Baraza linaboresha utaratibu wake wa kutoa motisha kwa Kamati hizi ili kuongeza morali ya utendaji kazi wa Mjumbe mmoja mmoja na hatimaye kwa Kamati nzima. Napenda kuwapongeza sana Wajumbe hawa kwa moyo wao wa kizalendo na utayari wa kujitolea waliouonesha katika kuitumikia jamii ya Watanzania. Jitihada za Wajumbe hawa zitachangia sana katika kuboresha utoaji wa huduma za nishati na maji nchini.

Sambamba na pongezi hizi, nitumie nafasi hii kulisihi Baraza kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati hizi ili ziweze kutekeleza vema majukumu yake na kama kuna changamoto

zozote za kiutendaji, Baraza lisisite kuwasiliana na Mdhibiti ili kuona ni kwa namna gani changamoto hizo kwa pamoja tunaweza kuzitatua.

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo,** Nimesikiliza kwa makini baadhi ya changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hizi. Nimeridhishwa na suluhu ya Baraza ya kuja na mbinu kufanya tathmini ya ufanisi wa kiutendaji kwa kila Mjumbe na hata Mpango wa Motisha kwa Wajumbe hao. Ni imani yangu kuwa, mbinu hizi zitaongeza tija na uwajibikaji wa wanakamati na hatimaye kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ndugu Mwenyekiti**, Wajumbe hawa ni miongoni mwa watu wachache ambao Baraza limewakabidhi dhamana kubwa katika kutetea watumiaji katika mikoa yao ambako ndiko watanzania wanakoishi. Hawa ndiyo wawakilishi wa EWURA CCC katika mikoa yao. Uwajibikaji na mshikamano wao ndiyo sababu pekee itakayowezesha watoa huduma za nishati na maji kutimiza wajibu wao wa kutoa huduma zenye ubora unaokubalika kwa watumiaji. Jambo hili halitawezekana kama wao wenyewe kama Kamati, hawatashirikiana katika utekelezaji wa majukumu yao. Ili haya yote yatekelezeke vyema, uwazi na kujitoa kwa dhati sharti viwe vipaumbele vyenu.

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo,** ninatambua kuwa, utekelezaji wa majukumu ya Baraza na Kamati hizi unahitaji

kufanya kazi kwa ukaribu na ushirikiano mkubwa na wadau wa Baraza. Kupitia hadhira hii, nipende kutoa wito kwa watoa huduma za nishati na maji kote nchini zikiwemo Mamlaka za Maji, TANESCO pamoja na vituo vya mafuta ambao ni miongoni mwa wadau wakubwa wa Baraza, kutoa ushirikiano wa dhati kwa Baraza na Wajumbe wa Kamati hizi za mikoa na kufanya kazi kwa kushirikiana katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Mdhibiti kwa upande wake ataendelea kutoa ushirikiano wa hali na mali wakati wote atakapopaswa kufanya hivyo, ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hizi na Baraza kwa ujumla. Kila mmoja akasimame katika sehemu yake kutekeleza wajibu wake. Ufanisi utapatikana kwa sisi sote kushirikiana**.**

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo**, nimeelezwa baadhi ya majukumu yanayotekelezwa na Wajumbe wa Kamati za EWURA CCC za mikoa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu haki na wajibu wa watumiaji, utaratibu wa kulalamika, kuhamasisha umma, na nyingine nyingi. Kazi hizi na nyingine nyingi zinazolenga kulinda na kumtetea Mtumiaji kama kazi ya msingi ya Baraza ni muhimu katika mstakabali wa kufikia malengo ya uwepo wa Baraza. Niwasihi mkajidhatiti kutoa elimu kwa jamii ili kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu haki na wajibu wao, hii itasaidia wao kufanya maamuzi na matumzi sahihi na endelevu ya huduma za nishati na maji na watachangia katika kuboresha huduma hizo hapa nchini.

EWURA inaunga mkono juhudi za Baraza na ipo tayari kushirikiana katika kuhakikisha maslahi ya watumiaji yanalindwa.

**Ndugu Washiriki wa Mafunzo,** ili mtekeleze majukumu yenu ya msingi yaliyopo mbele yenu, ni dhahiri mnahitaji kunolewa kwa kupatiwa elimu kwanza mfahamu nini mnatarajiwa mwenda kufanya na kazi hiyo inafanywaje. Ni kwa sababu hiyo leo hii mmekusanyika kwa umoja wenu chini ya uratibu wa Baraza kwa ajili ya kupatiwa mafunzo yatakayotolewa na wataalamu wabobevu kwenye sekta za nishati na maji. Niwasihi mkawe wasikivu na wenye utulivu wa kutosha wakati wa uwasilishaji mada mbalimbali zitakazokuwa zinatolewa, muwe wadadisi kupitia kuuliza maswali ili mwisho wa mafunzo haya lengo la mafunzo haya liwe limetimia, huku mkiwa tayari kwenda kutekeleza majukumu yenu.

Aidha, ninalisihi Baraza kuyafanya mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe hawa yakawe endelevu kwa kuwa, mambo mengi yanabadilika kila uchao. Kwa mfano kanuni mbalimbali zinarekebishwa na zingine kutengenezwa. Bila kuendana na wakati katika kujengeana uwezo, pengine tunaweza kujikuta tunatumia taarifa zilizopitwa na wakati na hivyo kupotosha umma. Kwa upande wa Mdhibiti, tutaendelea kulishirikisha Baraza kila kunapokuwa na mabadiliko, na pengine kuwa sehemu ya kuwajengea uwezo ili sote tuendane na wakati katika kumhudumia Mtanzania.

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo,** ni ukweli usiopingika kuwa bado Baraza linalo jukumu kubwa la uelimishaji katika maeneo mengi ya nchi yetu. Mathalan, nimearifiwa kuwa elimu inayotolewa inaishia kwenye maeneo ya Manispaa za mikoa tu kwa kuwa bado Kamati nyingi hazijaanza kufikisha huduma maeneo ya wilayani. Ni maelekezo yangu kuwa, Baraza liendelee kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuziwezesha Kamati hizi kupanua wigo wake wa utoaji elimu kufika hadi kwenye ngazi za wilaya.

Aidha, ni jambo lisilopaswa kubezwa kuwa bado watumiaji wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu haki na wajibu wao. Na hata wanapokuwa hawajaridhishwa na huduma zinazotolewa na watoa huduma, wengi wao wamekuwa hawaelewi ni wapi pa kulalamika, na ni mfumo gani watumie kuwasilisha malalamiko yao. Tumewashuhudia Watumiaji wengi wakipeleka malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji kwa wenyeviti na watendaji wa Kata na pengine kwa Wakuu wa Wilaya na hata Wabunge ama Polisi. Hali hii inaonesha kuwa, bado elimu kuhusu uwasilishaji wa malalamiko na utatuzi wake kwa upande wetu haijafikishwa kwa watumiaji ipasavyo.  Kupitia mafunzo haya ninawaagiza mkajikite katika kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi.

**Ndugu Mwenyekiti na Washiriki wa Mafunzo**, jambo la mwisho lakini si kwa umuhimu ninalotaka kuwasihi hapa ni kuhusu kusoma Sheria, Sera, Kanuni na Miongozo inayosimamia huduma za nishati

na maji. Hivi ni vitendea kazi muhimu kwetu sote. Bila kuwa na uelewa wa vitendea kazi hivi, dhana ya utetezi wa mtumiaji haitakuwa na maana yoyote. Inatupasa kutumia muda wetu kujielimisha katika haya ili kuinua kiwango chetu cha ufanisi wa kiutendaji.

Nawatakia mafunzo mema na kazi njema katika kipindi chenu cha utumishi. Tukishirikiana kwa pamoja, tunaweza kuleta mabadiliko chanya katika utetezi na uwakilishi wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji, na kuimarisha huduma hizo kwa kizazi chetu na vizazi vijavyo.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba **Mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za EWURA CCC yamefunguliwa rasmi, na**

**Asanteni kwa kunisikiliza!**